

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA MITIHANI  
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

664

**MITAALA NA UFUNDISHAJI**

**MUDA: Saa 3**

**2006/10/18 Asubuhi**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C.
2. Jibu maswali yote katika sehemu A, maswali **mawili (2)** kutoka sehemu B na swali **moja (1)** kutoka sehemu C.
3. Sehemu A ina alama 36, sehemu B ina alama 40 na sehemu C ina alama 24.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

**SEHEMU A (alama 36)**

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Fafanua dhana ya ukuzaji wa mitaala.
2. Jadili kwa kifupi hoja za wataalamu mbalimbali wanaomchukulia mwanafunzi kama msingi wa mitaala.
3. Tofautisha njia na mbinu za kufundishia na kujifunzia.
4. Orodhesha njia tatu (3) za utoaji wa mazoezi na mitihani kwa wanafunzi darasani.
5. Bainisha aina tatu (3) za mitaala.
6. Kipengele cha tathmini kina umuhimu gani katika andalio la somo?
7. Taja misingi mitatu (3) ya mitaala.
8. Kwa kutumia mifano halisi inayozingatia milango ya maarifa ya mwanafunzi, ainisha zana za kufundishia na kujifunzia.
9. Taja sifa za njia ya mhadhara kwa wanafunzi ambao ni watu wazima.

**SEHEMU B (alama 40)**

Jibu maswali mawili (2) kutoka sehemu hii.

10. Chagua somo moja linalofundishwa katika shule za msingi kisha andika andalio la somo kwa kuzingatia hatua zote muhimu.
11. Kwa bahati nzuri wewe ni mmoja wa walimu wanafunzi waliopangiwa mazoezi ya kufundisha ya muda mrefu. Jadili uzoefu wako katika mazoezi hayo ukionyesha faida uliyopata na mapungufu uliyoyaona.
12. Baada ya kumaliza mafunzo yako, umepewa nafasi ya kutoa semina kwa walimu walioko kazini ili kuwakumbusha namna nzuri ya kuandaa azimio la kazi. Taja vipengele muhimu utakavyovitilia mkazo na eleza umuhimu wa kila kipengele.
13. Fikiria na kisha jadili matatizo utakayoyapata iwapo utafundisha somo lako bila kuwa na azimio la kazi. Je matatizo hayo yanaweza kuleta matokeo gani kwa wanafunzi?

**SEHEMU C (alama 24)**

Jibu swali moja (1) kutoka sehemu hii.

14. Umepangiwa kufundisha darasa ambalo mwalimu anayekukabidhi anakutahadharisha kuwa darasa hilo lina wanafunzi wasio wasikivu, wenye fujo na hawamtii mwalimu. Jadili vipengele muhimu utakavyotumia ili kusaidia kudumisha nidhamu katika darasa hilo.
15. Eleza namna matumizi mazuri ya zana za kufundishia yanavyoweza kutatua tatizo la wanafunzi wengi kutoelewa somo/masomo wafundishwayo.
16. Jadili umuhimu wa kuhakiki mazoezi ya kufundisha ya muda mrefu.

Mweni  
Juma  
vipindi  
madakimu  
muda ndogo  
kazi ya mto  
kazi ya mto  
zana/vitaa  
Rejea  
kazi  
m  
matatizo  
hambonyu  
kazi za kazi